<INSERT DISTRICT OR SCHOOL INFORMATION & LOGO>

Ustahiki wa Mwanzo wa Usaidizi wa Ziada wa Lugha

SAMPULI YA BARUA YA TAARIFA YA MZAZI: Barua hii inatolewa na Idara ya Elimu ya New Hampshire kama aina ya Usaidizi wa Kiufundi kwa Mashirika ya Elimu ya Eneo (LEA) tunayosaidia. LEA zinaweza kuchagua kubinafsisha barua hii ili iendane na mipango ya eneo. Tunapendekeza sana kwamba LEA; ziweke tarehe ya barua, zipate saini, na zihifadhi nakala iliyotiwa saini katika faili ya jumla ya mwanafunzi.

Sampuli hii inajumuisha viwango vya chini zaidi vinavyohitajika chini ya *ESEA* §1112(e)(3) na (e)(4), 20 USC 6312 (2015) ili kukidhi masharti ya utiifu kwa taarifa ya mzazi. Barua ya taarifa ya mzazi lazima itolewe kwa wazazi wa wanafunzi wote wa EL ndani ya siku 30 za kalenda mwanzoni mwa mwaka wa shule au ndani ya siku 14 za kalenda baada ya mwanzo wa mwaka wa masomo.

Jina la Mwanafunzi:_____ Tarehe:_____
(mm/dd/yyyy)

Shule:_____ Gredi:_____

Mpendwa Mzazi au Mlezi:

Ulipomsajili mtoto wako shuleni uliombwa ujaze fomu ya Utafiti wa Lugha ya Nyumbani. Kwenye fomu hiyo ulisema kwamba lugha nyingine isipokuwa Kiingereza inazungumzwa nyumbani kwako. Kulingana na maelezo haya, shule ilimpa mtoto wako mtihani wa kupima Ufasaha wa Lugha ya Kiingereza (ELP) wa kimasomo. Madhumuni ya mtihani huo ni kubainisha kiwango cha ELP kwa wanafunzi wanaozungumza lugha nyingi ili kuhakikisha kuwa lugha si kizuizi katika kuelewa maudhui ya kimasomo ya kiwango cha gredi.

Tathmini ya ELP inayotumika katika New Hampshire ni Kichunguzi cha WIDA (WIDA Screener). Kama unavyojua, ukuzaji wa lugha ni mchakato unaoendelea kwa wote. Kichunguzi cha ELP hupima mahali mtoto wako yuko kwa sasa katika mchakato wa ukuzaji wa lugha ya Kiingereza. Ufafanuzi Kamili wa Utendaji kwa kila kiwango cha ufasaha wa lugha ya Kiingereza umejumuishwa kama kiambatisho cha barua hii kwa marejeleo yako.

Mtoto wako alipata alama ya jumla ya _____ kwenye kipimo cha 1-6. Unaweza kupata maelezo zaidi kwenye ripoti iliyoambatishwa ya alama.

1-Kuingia	2-Kuanzia	3-Kuendelea	4-Kupanuzi	5-Kuziba	6-Kufikia

Katika New Hampshire, mtoto yeyote anayepata alama za jumla za **4.4 au chini** anatambuliwa kama "mwanafunzi wa Kiingereza" (EL). Sheria ya shirikisho inahitaji shule za umma kutoa Mpango wa ziada wa Elimu ya Lugha ya Mafundisho (LIEP) au "mpango wa EL" kwa wanafunzi wote wanaostahiki huduma za lugha ya Kiingereza. Kulingana na matokeo ya mtoto wako ya mtihani **wa ELP, mtoto wako anastahiki huduma hizi**.

Kama mzazi/mlezi, mchango wako ni muhimu katika mchakato wa kufanya maamuzi. Una haki ya kisheria ya kuchagua mpango wa EL kati ya ile inayotolewa na shule au wilaya au kukataa huduma hizo. Hapo chini utapata muhtasari wa aina za mipango ya EL zinazopatikana kwa mwanafunzi wako.

Maendeleo ya Lugha ya Kiingereza: Mafundisho ya moja kwa moja ya lugha ya Kiingereza yanayolenga kukuza msamiati wa kimasomo. Mafundisho yanaweza kutokea darasani kama usaidizi wa “ndani ya darasa” au wanafunzi wanaweza “kuondolewa” darasani na kuwekwa kwenye kikundi kidogo au mafundisho ya 1:1 ambayo yanalenga malengo mahususi ya lugha.

Madarasa ya Maudhui kupitia EL Jumuishi: Walimu wa EL na wa darasani hushirikiana ili kutumia maudhui ya kimasomo kama njia ya kusaidia ukuzaji wa lugha darasani.

Mpango ya Ndani ya Kiingereza au Programu kwa Mgeni (SEI): Mipango iliyoundwa ili kukidhi mahitaji ya kimasomo na ya mpito ya wahamiaji wapya waliowasili au kwa Wanafunzi walio na Elimu Rasmi Iliyochache au Iliyokatizwa (SLIFE). Kwa kawaida, wanafunzi huhudhuria mipango hii inayojitosheleza kabla ya kuingia kwenye aina zingine mipango ya EL. Mara nyingi ili kuimarisha ustadi wa kimsingi katika maeneo ya maudhui, na pia mafundisho ili kuwafahamisha wageni na tamaduni na mazingira ya kielimu ya Marekani.

Lugha Mbili za Mpito: Mpango ambapo mafundisho ya maudhui yanatolewa kwa Kiingereza na lugha ya asili ya mwanafunzi. Mipango ya

lugha mbili inaruhusiwa kwa idhini ya awali kutoka kwa Bodi ya Elimu ya Jimbo la NH.

Lugha Mbili: Mpango wa kufundisha kwa lugha mbili kwa lengo la kusaidia wanafunzi wanapokuza ufasaha wa lugha katika lugha mbili. Wanafunzi hupokea mafundisho kwa Kiingereza na lugha nyingine katika darasa ambalo kwa kawaida huwa na nusu ya wazungumzaji wa Kiingereza cha msingi na nusu ya wazungumzaji wa lugha nyingine lengwa ya msingi. Mipango ya lugha mbili inaruhusiwa kwa idhini ya awali kutoka kwa Bodi ya Elimu ya Jimbo la NH.

Timu yetu inapendekeza kusaidia ukuaji wa Kiingereza wa mtoto wako kupitia mpango wa LIEP au EL unaonyeshwa hapa chini. Uwekaji kwenye mpango unaweza kubadilika kulingana na maendeleo ya mtoto wako. Shule itakuarifu kuhusu mabadiliko yoyote.

Mpango wa EL katika Wilaya	Uwekaji Unaopendekezwa na Wilaya	
☐	☐	Maendeleo ya Lugha ya Kiingereza ☐ Kuondolewa Darasani ☐Ndani ya Darasa ☐ Mchanganyiko
☐	☐	Madarasa ya Maudhui kupitia EL Jumuishi
☐	☐	Mpango ya Ndani ya Kiingereza au Programu kwa Mgeni
☐	☐	Lugha Mbili za Mpito
☐	☐	Lugha Mbili
	☐	Nyingine:

Tafadhali kumbuka, sheria ya shirikisho inawahitaji wanafunzi WOTE wa EL wafanye tathmini ya kila mwaka ya ufasaha wa lugha ya Kiingereza ili kupima maendeleo ya mwanafunzi katika kukuza ufasha wa lugha ya Kiingereza. Katika NH, mwanafunzi hufikia ufasaha anapopata alama za jumla za 4.5 au zaidi kwenye WIDA ACCESS au P2 kwenye mtihani wa Alternate ACCESS.

***Mzazi au Mlezi**: Tafadhali jaza sehemu hii na urudishe fomu nzima kwa shule ya mtoto wako. Nakala ya mwisho itahifadhiwa kwenye faili shuleni na nakala itatumwa nyumbani kwa rekodi zako pia.*

Tafadhali andika herufi za kwanza za majina:

	Ninafahamu alama za mtoto wangu za ufasaha wa lugha ya Kiingereza na ninaelewa ni kwa nini mtoto wangu alipendekezwa kwa mafundisho ya ziada ya lugha.
	Ninafahamu mipango ya EL ambayo shule inatoa.
	Ninaelewa kuwa mtoto wangu bado atahitajika kufanya tathmini ya kila mwaka ya ufasaha wa Kiingereza (yaani, mtihani wa "ACCESS"), hata nikikataa huduma za EL.
	Ninaelewa kuwa ninaweza kubadilisha uamuzi wangu wakati wowote katika mwaka wa masomo.
	Maelezo haya yamewasilishwa kwangu kwa lugha ninayoielewa kikamilifu.

☐ **Ndiyo**, Ningependa mtoto wangu ashiriki katika mpango wa EL unaoonyeshwa hapo juu kwa mwaka wa masomo wa _____.

☐ **Hapana**, Sitaki mtoto wangu ashiriki katika mpango wa wanafunzi wa Kiingereza katika mwaka wa masomo wa _____.

Jina la Mzazi au Mlezi:_____Saini: _____

Simu: _____Barua pepe: _____

Tafadhali wasiliana na mwalimu hapa chini, ikiwa una maswali yoyote.

<INSERT CONTACT INFORMATION>